**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU KLERRUU**

**SIMU:** 0765585195 - Mkuu wa Chuo

0719757543 -Makamu Mkuu wa Chuo

0754922608 -Msajili wa Wanachuo

Barua pepe: klerruutc@moe.go.tz

klerruutc@gmail.com

Chuo Cha Ualimu Klerruu
S.LP. 549,
**IRINGA**.

Jina.........................................................

**YAH: KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUMU YA UALIMU ELIMU YA MSINGI (SAYANSI NA HISABATI) MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya stashahada maalumu ya ualimu Elimu ya msingi **(**Sayansi na Hisabati**)** kwa mwaka wa msomo 2025/2026, **Hongera sana**. Hii ni nafasi muhimu kwako kwani wahitimu wa mafunzo haya wanatarajiwa kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati katika shule za msingi.

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **14/07/2025** bila kukosa. Kufika kwako kwa muda mwafaka kutakupa nafasi ya kushiriki katika mafunzo kabirishi yanayohusisha kufahamu kwa undani kuhusi kozi uliyochaguliwa, kuelewa sharia na taratibu za chuo na masuala mengine ya taaluma ya Ualimu kwa ujumla.
Unatakiwa kusoma kwa umakini na kuelewa maelekezo yote ya kujiunga na mafunzo. Unapaswa kuripoti chuoni kwa muda ulioelekezwa. Utapoteza nafasi endapo utashindwa kuripoti ndani ya **WIKI MBILI** tangu tarehe ya kuripoti chuoni.

Wazazi/Walezi na Wanachuo watatakiwa kujaza fomu ya makubaliano iliyoambatanishwa na kuwasilishwa chuoni siku ya usajili. Kila mwanachuo atatakiwa kufanyiwa vipimo vya afya katika hospitali ya Wilaya/Mkoa/Rufaa tu. Fomu ya majibu ya daktari uje nayo unaporipoti chuoni.
Nakutakia kila la kheri katika maandalizi ya kujiunga na chuo.

**…………………………………….**

**TUMAINI A. MANGILIMA**

**MKUU WA CHUO**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU KLERRUU**

Mahitaji ya kujiunga na chuo ni kama ifuatavyo;

**1. KUFUNGUA**

Muhula wa masomo utaanza tarehe **14/07/2025** kwa wanachuo wote wa Stashahada Maalumu ya Sayansi na Hisabati. Wanachuo wote wanatakiwa kuripoti chuoni muda wa kazi (kabla ya saa tisa na nusu mchana). Mafunzo kabirishi ni muhimu kwa wanachuo wote na yataanza mapema zaidi baada ya chuo kufungua.

**2. TAARIFA ZA CHUO**

**KILIPO**

Chuo cha Ualimu Klerruu kipo Mkoa wa Iringa – Manispaa ya Iringa Mjini. Kuna umbali wa wastani wa kilomita 2.5 toka ofisi za Makao makuu ya Posta mkoa wa Iringa, kipo pembezoni mwa barabara kuu ya Iringa – Dodoma – Mtaa wa Gangilonga katika kata ya Gangilonga.

**3. KAULI MBIU YA CHUO "Ufahamu na Ustadi ni Uhuru''**

**4. KOZI INAYOTOLEWA NA MUDA WA KOZI**

- **Kozi:** Stashahada Maalum ya Ualimu elimu ya Msingi (Sayansi na Hisabati)

**Muda wa mafunzo:** Miaka mitatu (3)

**4.1 YAHUSUYO KOZI**

Mafunzo ya Ualimu yanahusisha shughuli za kimtaala na zisizo za kimtaala katika mfumo wa Mihadhara, Semina, Mafunzo ya Ualimu kwa vitendo (MUV), Utunzaji wa mazingira, Michezo na fani mbalimbali.

**4.2 MAHITAJI YA MUHIMU YA KOZI**

Kila mwanachuo atatakiwa kuwasilisha katika ofisi ya Msajili kwa utambuzi vifaa vifuatavyo:

- Nakala mbili za muhtasari ya elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati
- Vitabu vya kiada vya shule ya msingi nakala moja kwa kila somo (Sayansi na Hisabati)
- Daftari kubwa 12 au zaidi (Counter book - Quire 3)
- Seti au mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set)
- Kikokotozi cha kisayansi (Scientific calculator)

**4.3 MAVAZI YA MICHEZO**

Kila mwanachuo atapaswa kushiriki katika michezo kwa kuzingatia ratiba ya chuo. Hivyo atapaswa kuja na mavazi yafuatayo kwa ajili ya michezo;

1. Trakisuti — Rangi ya bluu nyeusi (Dark Blue)
2. Wavulana - jezi za Juventus (full jersey - Pundamilia)

   Wasichana - jezi ya Manchester City (ya juu tu - Bluu bahari) na kaptula ya trakisuti

nyeusi (Min truck) inayoishia chini ya magoti

3. Raba za michezo
4. Soksi ndefu za michezo zenye ufito wa rangi nyeupe na bluu.

### 4.4 SARE ZA CHUO

- Kuanzia Julai 2008, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilirudisha utaratibu wa uvaaji wa sare maalumu kwa wanafunzi wa vyuo vya Ualimu. Sare za chuo chetu ni kama ifuatavyo;

- Suti pea mbili bluu-nyeusi (Dark blue) (koti na suruali/sketi Mbili na Tai ya bluu-nyeusi)
  - Suruali iwe na marinda mawili na upana chini uwe na **inchi 16**.
  - Sketi iwe ya rinda boksi, mifuko miwili na urefu iwe **inchi tano** kutoka katika goti.
  - Koti la suti liwe na vifungo viwili
  - Kwa wavulana koti liwe na mipasuo miwili nyuma
- Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari
- Viatu vya ngozi vya kamba rangi nyeusi (jozi mbili).
- Koti la maabara rangi nyeupe la mikono mirefu (Laboratory coat)
- Fulana yenye nembo ya Chuo utalipia Tsh. 15,000/= (Itapatikana chuoni)

**MUHIMU:**

- Wanafunzi wa kike wa dini ya kiislamu wataruhusiwa kuvaa vazi la "HIJAB" rangi ya bluu bahari.
- Maelekezo ya namna ya kupata sare za chuo yatatolewa mara ufikapo chuoni ili kuondoa utofauti baina ya wanachuo.

### 4.5 UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Kila mwanachuo anapaswa kuishi katika mazingira safi na salama. Ambapo atatakiwa kufanya usafi bwenini, karakana, darasani, maabara, ukumbi wa chakula, ukumbi wa mikutano na maeneo yote kuzunguka chuo.

## 5.0 USAJILI

### 5.1. UTAMBULISHO NA VIGEZO VYA KITAALUMA

Kila mwanachuo anaporipoti chuoni lazima aje vyeti vyake halisi kwa ajili ya uthibitisho na utambulisho.

Kama ifuatavyo;

- Barua na fomu ya kujiunga na chuo.
- Vyeti halisi vya kitaaluma (**sio nakala**).
- Cheti cha kuzaliwa.

- Cheti cha uchunguzi wa afya (Medical Examination Certificate) kilichothibitishwa na kupigwa muhuri kutoka katika hospitali Wilaya/Mkoa/Rufaa (Udanganyifu unaweza kukosesha huduma stahiki juu ya afya yako).

**ZINGATIA**:

- Toa Nakala nyingi za vyeti kwa matumizi binafsi ya baadaye.
- Kushindwa kuwasilisha nakala tajwa hapo juu siku ya usajili itakupelekea kutosajiliwa.

## 5.2. UCHANGIAJI WA GHARAMA

### 5.2.1.ADA

Gharama za mafunzo ya Ualimu zinachangiwa kwa kiasi fulani na serikali. Mwanafunzi atahitajika kulipa **ada ya kiasi cha Shilingi 450,000/=** kwa kila mwaka wa masomo. Kiasi hicho kitatakiwa kulipwa kwa mkupuo mara moja kwa mwaka au kulipwa kwa awamu mbili kwa mwaka wa masomo kwa kila mwanzo wa muhula wa masomo.

**Huruhusiwi kuripoti chuoni bila kiasi tajwa cha ada tajwa hapo juu**. Malipo ya ada yatahitajika kulipwa kwa kutumia mfumo wa malipo serikalini, baada ya kupata namba ya malipo **(CONTROL NUMBER)** kutoka kwa Mhasibu wa Chuo mara baada ya kuwasili chuoni. Mwanafunzi atatakiwa kuwasilisha nakala ya benki ya malipo ya ada (Bank pay-in slip) kwa ajili ya mchakato wa usajili.

### 5.2.2 MICHANGO MINGINE

- Mchango wa Serikali ya wanachuo 5,000/= (kwa mwaka)
- Huduma ya kwanza 10,000/= (kwa mwaka)
- Michezo 30,000/= (kwa mwaka)
- Kitambulisho na Usajili 20,000/= (mara moja)
- Mchango wa mahafali 10,000/=
- Usafi na utunzaji mazingira 20,000/= (kwa mwaka)
- Ulinzi 30,000/= (Kwa mwaka)
- Matengenezo 25,000/= (kwa mwaka)
- Godoro 10,000/= (kwa mwaka)
- BIMA ya Afya (NHIF) 50,400/= kwa mwaka (Lazima kwa wote wasiokuwa na bima ya afya)
- Ada ya Mtihani wa Taifa kwa mwaka wa wa tatu 50,000/=

Malipo yote ya michango yatatakiwa kulipwa kwa kupitia benki ya **NMB-Mkwawa** kwa akaunti namba **60501100006** Jina la akaunti **Mkuu wa Chuo, Chuo cha Ualimu Klerruu**. Mwanafunzi atatakiwa kuwasilisha nakala ya malipo siku ya usajili. Michango yote ni ya **LAZIMA** ili kukamilisha sifa za kusajiliwa.

**MUHIMU: Akaunti hii ni kwa ajili ya michango tu, ada ilipwe kwa kutumia Control number utakayopewa mara ufikapo chuoni.**

### 5.3.3 VIFAA

- Rimu moja isiyo na mistari (A-one).
- Soft bloom moja (1)

**5.2.3. HUDUMA ZA AFYA**
**NA MALAZI**

Kila mwanafunzi atahitajika kuja na vitu vifuatavyo kwa matumizi yake binafsi kwa ajili ya huduma za malazi na chakula: Mashuka mawili ya kutandika rangi ya bluu (kwa wavulana) na rangi ya waridi/pink (kwa wasichana), blanketi, chandarua, mto na foronya**. Magodoro yanapatikana chuoni kama iliyoanishwa kwenye sehemu ya michango.** Pia utatakiwa kuja na pazia rangi ya maziwa (cream) (wavulana) na nyeupe (wasichana).

Vitu vifuatavyo ni muhimu pia kuja navyo; Ndoo, sahani ya chakula, bakuli, kijiko, bilauri na kikombe. Pia uwe na chupa kubwa/kidumu cha kuhifadhia maji ya kunywa yaliyochemshwa. Unashauriwa kuja na hela kwa ajili ya matumizi binafsi. **Chuo hakitoi mlo maalumu kwa mwanafunzi yeyote**.

Wanafunzi wote wanatarajiwa kuzingatia usafi wa mwili na mazingira yake kwa kiwango cha hali ya juu. Uvaaji usio zingatia maadili ya Ualimu hautaruhusiwa kwa mwanafunzi yeyote.

**6.0. TARATIBU NA KANUNI ZA CHUO**

Taratibu na kanuni za chuo wakati wote wa mafunzo zitapewa kipaumbele katika kukujenga kuwa mwalimu mwenye haiba na tabia njema kwa jamii, na taifa kwa ujumla. Upendo, Amani na Uzalendo ni NGUZO muhimu katika maisha ya hapa chuoni. Utatakiwa kushirikiana katika kutumia huduma za jamii kama maji, umeme, na nyinginezo ikiwa ni pamoja na miundo mbinu mbalimbali ya Chuo. Pamoja na hayo chuo cha Ualimu Klerruu kinatoa nafasi sawa kwa wanafunzi wote kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na ujumuishi. Hivyo ninakutaka kutosita kujiunga na Chuo chetu. Hapa utapata elimu ya Ualimu kwa kiwango stahiki na kukuwezesha kuwa mwalimu mahiri.

**Taratibu na Kanuni za chuo utafafanuliwa kwa kina wakati wa mafunzo kabirishi na kuingia makubaliano ya kuziishi.**

## Karibu sana Chuo Cha Ualimu Klerruu.

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU KLERRUU**

FOMU YA MAKUBALIANO

KUKUBALI KANUNI ZA KUJIUNGA NA CHUO

Kwa Mkuu wa Chuo,
Chuo Cha Ualimu Klerruu,
S.L.P 549,
**IRINGA.**

SEHEMU 1: IJAZWE NA MWANAFUNZI

Mimi ______________________________________(Jina kamili), ninapenda kukujulisha kuwa nipo tayari kujiunga na chuo cha Ualimu Klerruu, na;

a. Nimesoma na kuelewa mahitaji yote kama yalivyoainishwa kwenye masharti ya kujiunga na chuo.
b. Nina ahidi kufuata na kutekeleza yote yaliyoainishwa kwenye masharti ya kujiunga na chuo. Ninatambua kuwa kushindwa kutekeleza hayo, nitawajibika na kukubali hatua za kinidhamu ambazo zitachukuliwa dhidi yangu.
c. Nina ahidi kushiriki ipasavyo katika shughuli za kitaaluma, kimichezo, shughuli za usafi na shughuli zote kadri ya ratiba ya chuo itakavyoniongoza.
d. Nina ahidi kutenda na kuonesha tabia njema ndani ya chuo na kuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kufuata sheria na taratibu za kazi ya Ualimu.
e. Nina ahidi kufika chuoni kwa tarehe za kufungua chuo zitakavyoonesha na kuleta mahitaji yote muhimu.
f. Nitarudi kwa wazazi/walezi/muajiri wangu kipindi cha likizo kwa anuani ifuatayo;

   Jina..................................................................
   Anuani ...............................................................
   Wilaya ...............................................................
   Mkoa ..................................................................
   Simu ..................................................................

Saini ya mwanafunzi_________________________________ Tarehe...............................................

SEHEMU ll: MZAZI/MLEZI MUAJIRI

Mimi ___________________________ (Jina kamili) ni mzazi/mlezi/muajili wa(Jina kamili la Mwanafunzi).

__________________________________________________________________

1. Ninathibitisha kuwa mwanafunzi aliyechaguliwa yupo chini ya usaidizi na uangalizi wangu. Ninakubali yale yote aliyoahidi kufuata. Nina ahidi kutoa msaada wa hali na mali kwa ajili ya kumsaidia kufanya vizuri katika masomo yake.
2. Nina ahidi kwamba mwanafunzi huyu atapata mahitaji yote ya vitu na fedha (Ada) ili kumuwezesha kusajiliwa na kumaliza mafunzo yake.
3. Nina ahidi kushirikiana na Uongozi wa chuo na jamii katika kumuwezesha mwanafunzi huyu kuwa na tabia na maadili mema yanayoendana na taaluma ya Ualimu.
4. Nitashirikiana na Uongozi wa chuo na jamii nzima katika kuchukua hatua stahiki katika kumjengea mwanafunzi tabia njema katika njia sahihi.

Jina ………………………………………………….. Anuani …………………………..

Wilaya ………………………. Mkoa ……………………….. simu………………………

Sahihi ……………

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

THE PRINCIPAL,
KLERRU TEACHERS' COLLEGE,
P.O.BOX 549, IRINGA
……….

TO: The Medical Office,

________________________

RE: MR/MRS/MISS

(Full name) ………………………………………………………………………………………

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for a full time to attend the course (Special Diploma in Secondary Education/Diploma in Secondary Education).

The examination should include the following;

**PART A**

a) Eye sight
b) Hearing
c) Limbs
d) Speech
e) Neuroses
f) Pregnancy
g) Mental and physical fitness
h) Venereal diseases
i) Leprosy
j) Peptic ulcers
k) Epilepsy
l) Tuberculosis

**PART B**

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full time teacher training course.

(a) Eye — sight ……

(b) Hearing……….

(c) Limbs …………

(d) Speech. …………

e) Venereal Disease.…

(f) Venereal disease……………………………………

(g) Leprosy………………………………………….

h) Peptic Ulcers……………………………….

(i) Epilepsy……………

(j) Tuberculosis………

(i) Neurosis.... . . . . . . . . . . . . . . . .. (ii) Mental and physical fitness ……………... (iii) Other serious disease ………

Date…………………………………Signature……………………………..Designation……………

Station . . . . . .... Official Stamp. . .